# KATA ZA MNINGA, NYOLOLO NA MADUMA
# MTIHANI WA KUJIPIMA DARASA – VII FEBRUARI 2022
# URAIA NA MAADILI

**SEHEMU A: ANDIKA HERUFI YA JIBU SAHIHI**

1. Kuna mifumo mikuu mitano katika mahakama. Mfumo wa ngazi ya juu kabisa ni -(A) Wa mwanzo (B) Wa Wilaya (C) Wa Hakimu mkazi (D)Wa Rufaa (E) Mahakama kuu
2. Zifuatazo ni tabia hatarishi ambazo hazipaswi kuigwa katika jami, ISIPOKUWA: (A) Utumiaji wa madawa ya kulevya (B) Ukahaba(C) Kutoa mimba (D) Ubakaji (E)Kutii kanuni na taratibu za Shule
3. Nchi yetu ina alama mbalimbali za Taifa. Ipi kati ya hizi zifuatazo ipo kwenye bendera ya Rais?(A)Mwenge wa Uhuru (B) Nembo ya Taifa (C) Bendera ya Taifa (D) Wimbo wa Taifa (E)Mnyama Twiga
4. Utunzaji wa mazingira ni jukumu la kila mtu. Pia kuna taasisi inayojihusisha na utunzaji huo ambayo ni;-(A)Taasisi ya Taifa ya utunzaji wa mazingira (NEMC) (B) Mamlaka ya mapato Tanzania (C) Wizara ya Afya (D) Shirika la chakula (E) Mamlaka ya hali ya hewa
5. Yafuatayo ni madhara ya ukeketaji kwa wanawake isipokuwa _______(A)Kupata heshima ndani ya jamii (B)Kutokwa na damu nyingi (C) Kifo (D) Maambukizi ya maradhi mbalimbali (E) Kupata matatizo wakati wa kujifungua
6. Mwanafunzi ana wajibu wakufanya yafuatavyo akiwa Shuleni ISIPOKUWA: (A) Kuandaa chakula kwa wanafunzi wenzie (B) Kufanya usafi wa darasa(C)Kuhudhuria mstarini (D) Kufanya kazi kwa bidii(E)Kuhudhuria vipindi
7. Upendo, Amani, Umoja, Ushirikiano na Uhuru hujulikanakama? (A) Demokrasia (B) Utandawaz (C) Tunu za Taifa (D) Nembo za Taifa (E) Rasilimali za nchi
8. ____ni mawe yenye thamani ambayo mara nyingi hupatikana chini ya ardhi. (A) Madini (B) Saruji (C) Udongo (D) Volkano (E) Mazao
9. Mkurugenzi ni Mtendaji mkuu katika Halmashauri. Je, katika Kata huwakilishwa na nani?(A)Diwani wa vitu maalum(B)Mkuu wa idara ya Elimu (C) Afisa Ugavi (D) Mwenyekiti wa Kata (E) Ofisa Mtendaji wa Kata
10. Kuna wanyama mbalimbali katika nchi yetu. Ni mnyama gani hutambulisha taifa letu? (A)Simba (B)Nyati (C)Twiga (D) Tembo (E) Swala
11. Ushirikiano ni hali ya kufanya kazi pamoja. Yapi ni matokeo ya kutowashirikisha wengine katika utekelezaji wa majukumu? (A) Maendeleo (B) Migogoro (C) Usawa (D)Uongozi (E) Umoja
12. Hamis na Jemina ni Watanzania wanaofanya kazi katika nchi ya China kwenye ubalozi wa Tanzania.Wakiwa huko China walioana na wakazaa mtoto aitwaye Macklin. Je, Macklin atakuwa raia wa namna gani atakaporudi Tanzania? (A)Raia wa China kwa kuzaliwa (B)Raia wa Tanzania kwa kurithi (C) Raia wa Tanzania kwa kuzaliwa (D) Raia wa China kwa kurithi (E) Raia wa China na Tanzania Kuoa au kuolewa ni haki ya kila mwanadamu. Hivyo kila binadamu ana haki ya kuoa au kuolewa na kuwa
13. na familia. haki hiyo ipo katika kundi gani?(a)Haki ya kisiasa (B) Haki ya kuishi (C) Haki ya jamii na kiuchumi (D) Haki ya Uhuru wa mtu binafsi (E) Haki ya kuamua ulitakalo
14. Shughuli mbalimbali za binadamu kuchangia uharibifu wa mazingira. Moja kati ya hizi huchangia uchafuzi wa vyanzo vya maji(A)Kuchoma misitu(B)Kutunza mazingira(C)Kupanda miti (D) Kufua nguo (E) Kulima kandokando ya vyanzo vya maji
15. Mihimili mikuu ya nchi ipo mitatu. Upi unatumika katika kutunga Sheria za nchi? (A) Baraza la madiwani (B) Serikali (C) Baraza la mawaziri (D) Bunge (E) Mahakama
16. Vyombo vya ulinzi na usalama vina kazi mbalimbali hapa nchini Je chombo gani hutumika kulinda mipaka ya nchi yetu?(A)Jeshi la kujenga Taifa(B)Jeshi la magereza(C)Jeshi la polisi (D) Jeshi la wananchi wa Tanzania (E) Usalama wa Taifa
17. Vyama vya siasa nchini vina kazi mbalimbali moja kati ya kazi hizo ni:(A) Kuhamasisha maandamano ya uvunjifu wa Amani (B)Kuitisha mikutano ya hadhara tu (C) Kuhamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo (D) Kuomba kura kwa wananchi (E) Kutumia mali za umma
18. Ni muhimu kutoa elimu ya afya ya uzazi katika jamii. Hii husaidia;-(A)Kupunguza mimba za utotoni (B) Kukuza tabia hatarishi (C) Malezi mabaya (D) Ongezeko la watoto wa mitaani(E)Kuongeza wataalam mbalimbali
19. Nchi nyingi Kiafrika zilipata Uhuru kupitia vyama vya siasa. Chama kipi kati ya hivi vifuatavyo kiliongoza Mapinduzi ya Zanzibar___ (A) Z P P P (B) Z N P (C) C C M (D) A S P (E) TANU
20. Uchaguzi wa Rais, Wabunge na madiwani hufanyika kila baada ya miaka mitano. Kwa mara ya mwisho Tanzania ilifanya uchaguzi

mwaka ____ (A) 1995 (B) 2020 (C) 2015 (D) 2010 (E) 1992

21. Jamhuri ya muungano wa Tanzania ilipatikana tarehe 26.4.1964. Hii ilitokana na muungano wa nchi mbili ambazo ni ______ (A) Tanzania na Zanzibar (B) Tanganyika na Zanzibar (C) Tanganyika na Tanzania (D) Unguja na Tanganyika (E) Unguja na Pemba
22. Uhusiano mzuri ni muhimu katika jamii. Urafiki ni kati ya uhusiano. Lipi kati ya yafuatayo hutambulisha wema? (A) Kuishi eneo moja(B)Kusoma shule moja (C) Tabia njema na upendo (D) Kulala pamoja (E) Kuvaliana nguo
23. Ni wajibu wa kila raia kushiriki shughuli za maendeleo ya jamii . Ushiriki katika shughuli hizo hupelekea: (A) Umaskini (B) Uwoga na kutokuwa na usalama (C) Uzalendonamshikamano (D) Utengano (E) Migogoro
24. Ushirikiano wa kimataifa una faida lakini unaweza kuwa na changamoto kama vile –(A) Uhamiaji haramu (B) Ujenzi wa miundombinu (C) Kukuza biashara (D) Ushirikiano mzuri na mataifa jirani (E) Kulinda amani
25. Kuna njia mbalimbali za kuhamashisha jamii katika kutoa misaada. Njia isiyo sahihi ni: (A) Makongaman (B) Mitandao ya Jamii(C)Vyombo vya habari (D) Ushauri nasaha (E) Vipeperushi
26. Kwa mara ya kwanza mwenge wa uhuru uliwashwa katika mlima Kilimanjaro mwaka 1961 na kaptani aliyeitwa _____ (A) Mwl. Julius Nyerere (B) Alexander Nyirenda (C) Seti Benjamini (D) John Malecela (E) Cleopa Msuya
27. Shujaa aliyeunganisha makabila mengi ili kupigania uhuru wa himaya yake kusini mwa Tanzania alijulikanakama (A) Kinjeketile Ngwale (B) Chifu Mangungo (C) Mangi sina (D) Chifu Mkwawa (E) Chifu Isike
28. Kwenye nchi ya kidemokrasia ustahimilivu wa kisiasa ni msingi wa demokrasia. Hii ni muhimu kwa sababu;-(A)Inasaidia washindi kushinda bila kampeni (B) Inaleta maelewano kati ya washindani (C) Inasaidia kunyamazisha wafadhili (D) Inasaidia kuwaridhisha wafadhili (E) Inaruhusu kutangaza washindi wa upande wao
29. Utamaduni ni kipengele muhimu katika umoja wa mataifa. Shirika linalojihusiha katika utamaduni ni : (A) UNHCR (B) WHO (C) FAO (D) UNESCO (E) ILO
30. Tanzania ni nchi yenye uhusiano mzuri na nchi mbalimbali Africa. Uhusiano huu umekuwa kutokana na? (A) Utunzaji wa mazingira (B) Jumuia zilizopo (C) Uhusiano wa kimichezo (D) Utamaduni (E)Utandawazi
31. Abeid Aman Karume ni Rais wa kwanza wa Zanzibar, aliuwawa na maadui wa maendeleo lini? (A) 14.10.1999 (B)7.4.1972 (C) 17.3.2021 (D) 12.4.1984 (E)12.1.1964
32. Usafi ni muhimu kwa afya ya binadamu . Unaposhauriwa kuosha mikono kwa maji safi na sabuni husaidia kujikinga na : (A) Kipindupindu na taifodi (B) Taifodi na malaria (C) Kipindupindu na kifua kikuu (D) Malaria na kifua kikuu (E) Kaswende na tetenasi
33. Mojawapo ya hizi zifuatazo ni athari za kutofikiri kwa uyakinifu –(A)Kufanya mambo kwa mpangilio (B) Kushindwa kufikia malengo (C) Kutatua changamoto zinazojitokeza (D) Kukabiliana na hatari za maisha (E) Kubaini changamoto kwa urahisi
34. Ni muhimu kujiunga na klabu za masomo shuleni ili kuendelea kujifunza. Moja ya faida ya kujiunga na klabu hizo ni: (A) Kukuza uelewa na migogoro (B) Kukuza uelewa nakujiamini (C) Kushindana kwa majibizano (D) Kuwa maarufu na kuvuja haki za binadamu (E) Kushindana na Walimu kimasomo
35. Utamaduni ni jumla ya mambo yote katika maisha ya mwanadamu, unajumuisha vipengele mbalimbali. Hata hivyo kimoja kati ya vifuatavyo siyo sahihi A. Rangi (B) Lugha (C)Dini (D) Mavazi (E) Sanaa
36. Zifuatazo ni jumuiya za kimataifa ambazo Tanzania ni mwanachama isipokuwa moja ambayo ni: A) Jumuiya ya Afrika Mashariki (B) Jumuiya ya Kusini mwa Africa (C) Umoja wa Mataifa(D)Jumuiya ya Afrika Magharibi (E) Jumuiya ya madola
37. Rushwa ni adui wa haki. Moja kati ya hizi zifuatazo si athari za rushwa katika jamii yetu;-(A)Serikali kushindwa kufikia malengo (B) Kuongezeka kwa gharama za kiutawala (C) Kukosekana kwa ujasiri (D) Kuongezeka kwa vitendo viovu (E) Kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato
38. Mchakato wa ujifunzaji mafunzo na ufundishaji hasa mashuleni na vyuoni unaosaidia kuboresha elimunakukuza ujuzi huitwa: (A) Uadilifu (B) Kujitambua (C) Uhuru (D) Utu (E) Elimu
39. Tanzania ni nchi yenye amani lakini mwaka 1978 – 1979 ilipigana na nchi ya _________ (A) Kenya (B) Rwanda (C) Uganda (D) Zambia (E) Msumbiji

**40.** Wakimbizi ni raia waliokimbia nchi zao kutokana na sababu mbalimbali. Idadi kubwa ya wakimbizi waliopo Tanzania wametokana na ______(A)Njaa (B) Vita vya wenyewe kwa wenyewe (C) Athari za mafuriko (D) Ukame (E) Jangwa

**SEHEMU B**

41. Orodhesha kazi mbili za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (a) ______ (a) ______
42. Serikali ya watu iliyowekwa na watu kwa manufaa ya watu ni ______________________
43. Mtu anayeishi nchi fulani na kuwa na haki zote anaitwa ______________________________
44. Kauli mbiu ya Tanzania iliyopo kwenye nembo ya Taifa ni _____________________________
45. _______ ni Sheria kabla haijatiwa saini na Rais.